

CHANGAMOTO



Wanafunzi wa shule ya msingi wakigombea kupanda usafiri wa daladala ili warejee nyumbani kwao. Picha na Maktaba Wakigombea kupanda usafiri wa daladala ili warejee nyumbani kwao. Picha na Maktaba

Tuzo Mapunda, Mwananchi
tmapunda@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Matukio ya unyanyasaji unaofanywa kwa wanafunzi kwenye vyombo vya usafiri, yanaweza kukuliza.

Ni matukio ya miaka nenda rudi ambayo aghalabu hugubikwa na chuki, vilio na hata mapambano kati ya wanafunzi, wazazi na makondakta.

Ndani ya simulizi ya matukio haya, uzoefu unaonyesha kutokuwapo kwa dhamira ya dhati ya kumaliza 'vita' kati ya wanafunzi na makondakta wa daladala katika maeneo mengi nchini.

Hata hivyo, habari njema ni kuji-tokeza kwa Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa aliyeagiza Mamlaka ya Udhidhi Usafiri Ard-hini (Latra) kuwaadhibu madereva na makondakta wa daladala wana-owanyanyasa wanafunzi.

Profesa Mbarawa alitoa maelekezo hayo kwa mamlaka hiyo jana, kati-ka mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dodoma.

Msingi wa agizo lake ni malalamiko ya mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Jangwani jijini Dar es Salaam, aliye-andika barua kulalamikia kubaguli-wa na makondakta wa daladala kwa kuwa hawalipi nauli kamili.

Kwa mujibu wa barua hiyo iliyo-onukuliwa na Profesa Mbarawa, wanafunzi inawalazimu kusima-ma barabarani kwa muda mrefu wakububiri usafiri, wanaelewa kufika shuleni na wakati mwingine wanashindwa kabisa kufika.

Profesa aliielekeza Latra kuhaki-kisha uthibitishaji wa madereva na usajili wahudumu kwenye mabasi, huku ikitoa adhabu kali kwa madere-va na makondakta watakabainika kuwanyanyasa wanafunzi.

Aliagiza Latra kuhakikisha treni za abiria, daladala zote nchini na mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani zimeandikwa namba za bure ili abiria wapige wanaponyanyaswa, huku Polisi wakifanya ukaguzi wa mara kwa mara vituoni.

Hata hivyo, alisema mikakati ya Serikali ni kuanzisha huduma za mabasi maalumu yaendayo haraka kwa ajili ya wanafunzi, hususan asu-buhi na jioni.

Hatua nyingine alisema ni kute-nga mabehewa maalumu kwa ajili ya wanafunzi kwenye treni za mijini (Dar es Salaam), ili kupunguza mson-gamano, kuongeza usalama na kutoa unafuu wa usafiri kwa wanafunzi.

Kero usafiri kwa wanafunzi mijini, tunakwama wapi?

"Kurasimisha na kusimamia utoza-ji wa nauli maalumu ya Sh200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala, kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata huduma hizi kwa gharama nafuu," alisema.

Walichosema makondakta, madereva

Hata hivyo, baadhi ya makondakta na madereva walidai kuwa, mazingi-ra ya biashara yanawalazimu kubana wingi wa wanafunzi kwenye vyombo vyao.

Wadau hao wa usafiri wa daladala, walisema kabla Serikali haijachukua hatua, inapaswa kufanya utafiti kubaini uhalisia wa tatizo, kwa kuwa shida haipo kwa makondakta na madereva pekee, wakati mwingine hata wanafunzi ni tatizo.

Walisema baadhi ya wanafunzi wanachagua kupanda daladala zenye muziki pekee, wengine wakikaa kwenye viti wanagoma kuwapisha watu wazima, ilhali nauli wanazolipa ni chini ya nusu ya inayolipwa na mkubwa.

Kwa mujibu wa Chama cha Kute-tea Abiria (Chakua), tatizo ni kubwa, huku kikitahadharisha kuwa, ili hatua zichukuliwe kunahitajika uchun-guzi wa kina, utakaohusisha wadau wote.

Mmoja wa viongozi wa juu wa Umoja wa Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam (Darcoboa), aliyeomba hifadhi ya jina lake, alisema kabla ya Serikali kutoa adhabu, kufanyike utafiti wa kina kupata uhalisia wa tatizo.

Alisema wanafunzi wanaowahi kufika vituoni, hususan asubuhi, mara nyingi hupata huduma, laki-ni kutokana na wingi wa abiria na mahitaji ya kibiashara, wahudumu hulazimika kuzingatia mapato yan-ayoingia.

"Wanafunzi wanaowahi kwenye vituo wanahudumiwa, lakini muda wa biashara ukiwa na wateja wengi ni lazima uangalie hesabu inayoingia,"

alisema.

Katika mazingira ambayo baadhi ya abiria hulipa nauli ndogo (Sh200) huku wengine wakitakiwa kulipa nauli kubwa, alisema kipaumbele lazima kitatolewa kwa wanaolipa zaidi.

"Kuna mambo mengi ya kuzin-gatia. Mbona mabasi ya wanafunzi yanatoza nauli kubwa, lakini hiyo imefanyika kwa mipango maalumu iliyowekwa kwa ushirikiano na wazazi," alisema.

Hata hivyo, alisema wazo la kubeba wanafunzi wengi kwa wakati mmoja katika mazingira ya usafiri na miun-dombinu ya Jiji la Dar es Salaam ni gumu kutekelezeka na linaweza kus-ababisha hasara kwa waendeshaji.

"Hatukatai kubeba wanafunzi, lakini Serikali izingatie daladala ni biashara kama biashara nyingine, tunalipa kodi. Malalamiko ya wana-funzi yalipaswa kufanywa utafiti na kutafutiwa suluhu badala ya kulau-mu daladala," alisema.

Alisema kuna maeneo ambayo daladala hubeba wanafunzi wengi pale ambako hakuna abiria wen-gi, mfano Kigamboni, lakini kati-ka baadhi ya maeneo wanafunzi huachwa kutokana na umbali mfupi wa wanapokwenda.

"Pia, inapaswa wawe na nauli kamili kwa sababu chenji siku hizi hununuliwa. Kilichofanyika ni kuwa-chonganisha wafanyabiashara na Serikali, ilhali utafiti ungefanyika kwanza kubaini ukweli wa jambo hilo," alisema.

Dereva wa daladala mkoani Dar es Salaam, Abdallah Said alisema kazi ya udereva ni sawa na kazi nyingine yoyote na madereva wanalazimi-ka kuheshimu masharti ya wajiri wao, ikiwamo kufikisha hesabu zin-azotakiwa, la siyvo hupoteza ajira.

Alisema dereva anaweza kulazimi-ka kuacha kazi endapo atashindwa kukidhi kiwango cha hesabu kinacho-takiwa na mmiliki wa chombo, hata kama sababu ni kubeba wanafunzi.

"Mimi ni binadamu nafanya kazi hii. Sipendi kumuacha mtoto nji-

ani wala siwezi kufurahia, tena mwenyewe nina watoto. Laki-ni inafika wakati, hasa asubuhi na jioni, wanafunzi ni wengi na wateja ni wengi. Unafungua biashara asubuhi na jioni unat-akiwa kufunga hesabu unafany-aje?" alihoji.

Haja ya utafiti

Mwenyekiti wa Umoja wa Makondakta kutoka Mkoa wa Mwanza, Self Nassor alisema ni muhimu utafiti ufanywe kwa sababu hata wanafunzi wanach-agua gari ya kupanda.

"Wengi wanataka kupan-da magari yenye muziki na yale ambayo hayana muziki hawapandi na wengine wanalipa nauli kamili na wanakaa kwenye siti," alisema.

Katibu Mkuu wa Chakua, Hashim Ramadhan alisema wamekuwa wakikumbana na migogoro hiyo mara kwa mara.

Alisema makondakta wame-kuwa wakilazimisha wana-funzi kulipa kati ya Sh500 hadi Sh700, na wanafunzi wasikuwa na kiasi hicho hunyimwa usafiri.

Alisema wasichana ndio waathirika wakubwa zaidi wa hali hiyo, akisema baadhi yao hutoka shuleni saa tisa alasiri lakini hufika nyumbani hadi saa tatu usiku kutokana na kusubiri usafiri kwa muda mrefu.

Walichokisema wazazi

Juma Selim, mzazi wa mwa-nafunzi jijini Dar es Salaam, alisema amewahi kumpokea mwanaye akiwa na jeraha lili-losababishwa na kusukumwa na kondakta, wakati akigombea daladala.

"Mtoto alikuwa anapambana apande, kondakta anamsukuma asipande wapande wakubwa kwa sababu nauli ya mwanafun-zi ndogo, akaanguka akaumi. Kuna mengi wanakutana nayo watoto. Serikali isimame hasa kuwalinda wanafunzi," alisema.

Mzazi mwingine, Neema Mol-lel mkazi wa Arusha alisema imekuwa kawaida mwanawe kumsimulia vituko vya makon-dakta kila siku anaporudi kutoka shuleni.

"Mwanangu ananiambia hawaruhusiwi kupanda hadi daladala iwe imejaa kwanza. Sasa ikijaa mtoto mfupi anaumi sana anakosa pumzi ni mateso wanateseka. Wengine wana wakataa. Mwanangu anato-shuleni saa 10 lakini nyumba anafika saa moja usiku, waki-ti alipaswa afike saa 11 jioni alisema.

Dawa ya tatizo

Bakari Heri, mwalimu mstaari alisema pamoja na kutokuwaji kwa mkakati maalumu kusai-ia wanafunzi, anashauri Se-ri-kali kwa kutumia vyombo kar-manispapa, wilaya na halmasha-ri, kuweka mikakati ya kusafi-sha wanafunzi.

"Lakini hata shule nazo z-aweza kujiongeza kama ilivyo-nyika kwa baadhi ya shule am-zo wazazi na walimu wan-akubaliana kukodisha mab- maalum. Tena shule hizi ni umma," alisema Heri.

WALIMU WANENA

Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Suleiman Ikomba alisema kuwaacha wanafun-zi barabarani bila usafiri wa kwenda au kurudi shuleni si jambo jema na lina madhara kwa Taifa. Alisema kuna haja kwa mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kushughu-likia suala hilo, kwa busara za kawaida si sahihi kuwaacha wanafunzi barabara-ni, hasa wanapoku-wa wanawahi kufika shuleni.

"Kwa macho ya kawaida ya ndani, si jambo jema kuona watoto wanaachwa barabarani na maba-si wakati wanataki-wa kuwahi shule," alisema.

Ikomba alisema kuchelewa kwa mtoto kufika shuleni au kurudi nyum-bani kunamuathiri kisaikolojia, hasa ikizingatiwa mtoto anaishi kwa kutege-me watu wazima.

"Hatuwezi kujenga kizazi kinachochukia wafanyabiashara wa magari tangu wakiwa wadogo kwa sababu ya kuachwa njiani."

Alisema jambo hilo si madereva wa daladala pekee, bali pia kwa watu bin-afsi wenye vyombo vya usafiri, kubeba jukumu la kuwasaid-ia wanafunzi pale inapowezekana.

Student's viral appeal sparks govt action on commuter bus abuse

By Julius Maricha
@TheCitizenTz

news@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. The government has ordered transport regulators and police to strengthen enforcement against public transport operators accused of denying students access to commuter buses, following a viral appeal by a form one student highlighting widespread mistreatment.

The minister for Transport, Prof Makame Mbarawa, on February 4, 2026, said the authorities had taken seriously a video circulating on social media in which a student, identified as Mariana Eric Mirindima of Jangwani Secondary School, described the challenges faced by students who rely on commuter buses (daladala) to get to school.

In her letter, the student said conductors often refuse to carry students because they pay a subsidised fare, forcing many to wait for long hours, arrive late at school or miss classes altogether.

She warned that the situation exposes students to safety risks and undermines their right to access education.

Addressing journalists in Dodoma on Wednesday, February 4, 2026, Prof Mbarawa commend-

ed the student and her parent for speaking out, saying the government had listened and would act.

"The voice of students has been heard and will be acted upon," said the minister, adding that the incident reflects a broader problem that requires firm enforcement of existing transport laws and regulations.

Prof Mbarawa said the government, through the Land Transport Regulatory Authority (Latra), would take action against bus owners, drivers, and conductors found violating rules governing student transport, regardless of their status.

He reiterated that while the private sector provides public transport services, the government retains oversight to ensure services are delivered in a safe, fair, and dignified manner.

As part of efforts to improve student transport in urban areas, the minister outlined several measures already in place, including the introduction of special rapid buses for students during morning and evening peak hours, as well as the allocation of dedicated carriages for students on Dar es Salaam's commuter trains.

He also reaffirmed that the official student fare of Sh200 applies to both rapid buses and daladala



The minister for Transport, Prof Makame Mbarawa, addresses the media during a recent conference.

PHOTO |
THE CITIZEN
CORRESPONDENT

services, warning operators against charging more or refusing service.

In addition, the government is enforcing laws requiring the certification of drivers and the registration of conductors, a move aimed at improving professionalism and accountability in the public transport sector.

To strengthen implementation, Prof Mbarawa directed Latra to fast-track the verification of drivers and registration of conductors in all towns and cities, and to impose strict penalties on those found harassing or discriminating against students. Latra has also been instructed to enhance moni-

toring of student fares, service standards, and safety, while stepping up public education campaigns so both operators and passengers understand their rights and obligations.

The minister said all daladala, commuter trains, and upcountry buses must display toll-free numbers to allow passengers to report abuse. Students and members of the public can report incidents through Latra's toll-free lines or via WhatsApp by submitting photo or audio evidence.

He added that Latra will work closely with the police to conduct regular and surprise inspections at bus stops, par-

ticularly during morning and evening hours, to ensure students are transported safely.

Prof Mbarawa called on the public to play an active role in protecting students from mistreatment, stressing that safeguarding children in public transport is a shared responsibility. He also urged daladala owners to remind their employees to comply with the law, warning that violations would attract punitive action.

"The government remains committed to building a public transport system that protects the rights, safety, and welfare of students and all citizens," the minister said.

USAFIRI

Na Waandishi Wetu

KAULI ya serikali ya kutaka kuanzisha mabasi maalum yaendayo haraka pamoja na kutenga mabehewa maalum ya treni za mijini kwa ajili ya wanafunzi jijini Dar es Salaam, ilipokewa kwa kicheko miongoni mwa baadhi ya wadau wa usafiri.

Wengi wao wakionesha matumaini mapya ya kumalizika kwa adha ya muda mrefu ya wanafunzi kukosa usafiri wa uhakika.

Kicheko hicho kilitokana na uzoefu wa miaka mingi wa ahadi ambazo, kwa mtazamo wa baadhi ya madereva na makondakta wa daladala, hazijawahi kutekelezwa ipasavyo, hasa katika suala la ulinzi wa haki za wanafunzi katika usafiri wa umma.

Hata hivyo, serikali imesisitiza kuwa safari hii imejipanga kikaamilifu kuhakikisha mpango huo unatekelezwa kwa vitendo.

Akizungumza jana jijini Dodoma na waandishi wa habari, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema serikali inakusudia kuanzisha huduma hizo mahsusi kwa wanafunzi kama sehemu ya mkakati wa kuboresha usafiri wao, kupunguza msongamano wa abiria na kuimarisha usalama.

Alisema lengo kuu ni kuhakikisha wanafunzi wanafika shuleni na kurejea majumbani kwa wakati na kwa usalama, bila kudhalilishwa au kunyimwa haki yao ya msingi ya usafiri.

"Serikali imesikia kilio cha wanafunzi. Tunataka kuwapa unafuu wa usafiri kwa gharama

Kicheko usafiri kwa wanafunzi

"Serikali imesikia kilio cha wanafunzi. Tunataka kuwapa unafuu wa usafiri kwa gharama nafuu na mazingira salama, ili waendelee na masomo yao bila vikwazo," Profesa Mbarawa

nafuu na mazingira salama, ili waendelee na masomo yao bila vikwazo," Profesa Mbarawa alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, umuzi huo umetokana na barua iliyoandikwa na Mariana Mirindima, mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Jangwani, na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii, akieleza changamoto wanazokutana nazo wanafunzi wanapotumia daladala jijini Dar es Salaam.

Katika barua hiyo, Mariana alieleza kuwa baadhi ya makondakta wamekuwa wakigoma kuwabeba wanafunzi wakidai hawalipi nauli kamili, hali inayowalazimu kusimama vituoni kwa muda mrefu, kuchelewa kufika shuleni au hata kushindwa kabisa kuhudhuria masomo.

Prof. Mbarawa alisema serikali inalenga kurasimisha na kusimamia ipasavyo utozaji nauli maalum ya Sh. 200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala, kwa mujibu wa taratibu zilizopo, ili kuondoa mianya ya manyanyaso.

Vilevile, aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi (LATRA) kuharakisha zoezi la kuthibitisha madereva na kusajili makondakta katika miji yote nchini, pamoja na kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watakabainika kuwanyanyasa wanafunzi.

Aliongeza kuwa LATRA, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, pia inapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushitukiza katika vituo vya daladala, hususan nyakati za asubuhi na jioni, kuhakikisha wanafunzi wanapata usafiri bila bughudha.

Baadhi ya madereva wa daladala

jijini Dar es Salaam wameibua hoja tofauti wakidai kuwa wanafunzi nao huchangia changamoto hizo kwa kuchagua magari ya kupanda, hususan yale mapya yenye muziki na intaneti, na wakati mwingine kusumbua ulipaji nauli.

"Unawakuta kituoni wapo wengi, lakini wanakataa kupanda gari eti halina muziki au WiFi. Sisi pia tunafanya biashara," dereva aliyejitambulisha kwa jina la Alfaleti Mwambona alisema.

"Ni kweli hatupendi kupakia wanafunzi wengi zaidi ya 10 kwa wakati mmoja, hasa nyakati ambazo abiria wengine pia ni wengi. Lakini hatuwaachi kabisa, tunawaomba wasizidi idadi hiyo," alisema.

Mwambona aliongeza kuwa changamoto kubwa hujitokeza pale wanafunzi wanapokuwa wengi kituoni na kutaka kupanda wote kwa pamoja, jambo ambalo huwa gumu kwa madereva wanaotakiwa kufikisha hesabu kwa wamiliki wa magari, kununua mafuta na kujipatia kipato cha kujikimu.

Kwa mujibu wa Mwambona, nyakati za jioni hali huwa tofauti zaidi kwani baadhi ya wanafunzi huchagua magari wanayotaka kupanda badala ya kukubali gari lolote lililopo.

"Unaweza kufika kituoni saa 10 jioni, abiria wachache, unawaambia waingie, wanakataa wakisema gari bovu, halina muziki au halina intaneti. Wanayajua magari yote -mapya, yenye muziki na yale wanayodai ni mabovu," alisema.

Alisema wakati mwingine madereva huwahitaji wanafunzi wapande

mapema ili kupata fedha ndogo ndogo za chenji, lakini wanafunzi huchelewa makusudi na kucheza vituoni hadi abiria wanapoongezeka.

Dereva mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Abel, alisema baadhi ya wanafunzi hata mchana hukataa kupanda daladala na badala yake huomba msada katika magari binafsi au bodaboda.

Alisema pia changamoto ya ulipaji nauli ni sababu nyingine inayowafanya madereva kuwa waangalifu kubeba wanafunzi wengi.

"Unampandisha mwanafunzi, ukimda nauli anakwambia anaipata kwenye begi, anatafuta hadi anashuka. Wengine wanasema wamepoteza. Ndiyo maana tunasisitiza atoe nauli kabla hajapanda," Abel alisema.

Hata hivyo, wanafunzi wamesema wanapitia madhila makubwa ikiwa mo kusimama vituoni kwa saa mbili hadi tatu, kudhalilishwa na kutukana na wakati mwingine kunyimwa usafiri kabisa.

Gilbert Shayo, mwanafunzi wa Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari Tambaza, alisema mpango wa serikali ukitekelezwa kikamilifu utapunguza kwa kiasi kikubwa mateso wanayokumbana nayo.

"Kama haya mabasi yataletwa na yakawa maalum kwa wanafunzi, yatakuwa mkombozi mkubwa. Tunachotaka ni ratiba nzuri na ya uhakika," Shayo alisema.

"Imeandaliwa na Rehema Matowo (DODOMA), Elizabeth Zaya na Sagini Hamis (DAR)

The Guardian February 5, 2026 pg 1

Govt plans special rapid bus service to transport to school

SPECIAL CITY PUPIL

transport to school

SKIP SAFETY RISK

By Polycarp Machira, Dodoma

THE government has unveiled new measures to improve pupil transportation in urban areas, including the introduction of special rapid buses dedicated to pupils during morning and evening peak hours, especially in Dar es Salaam.

Prof. Makame Mbarawa, the Transport minister, announced these plans at a press conference here yesterday, following concerns over incidents of pupils' mistreatment by some commuter bus crew.

Mariana Mirindima, a Form One pupil at Jangwani Secondary School in Dar es Salaam, was shown in recent social media video said the video that some conductors refuse to pick up pupils as they pay reduced fares.

The situation forces many pupils to wait for extended periods at bus stops, causing lateness at school and, in some cases missing classes altogether, she said, similarly citing safety concerns as pupils stranded along roads are exposed to various risks.

It undermines their right to access education in a safe environment, the activist video noted, with the minister commending the video initiative by the pupil and her parent for raising the issue before the broad public.

Describing the move as an example of responsible civic engagement, he assured the public that the government had listened to the concerns and would take appropriate action. "The voice of pupils has been heard



President Samia Suluhu Has
Future of Investment: An Afr
State House

Samia rankin

TURN TO PAGE 2

Latra yapewa maagizo usafiri wa wanafunzi

Na Ikunda Erick, Dodoma

SERIKALI imetoa maagizo kwa Mamlaka ya Udhidhi Usafiri Ardhi (LATRA) ili wanafunzi wasinyanyaswe katika vyombo vya usafiri.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema kwenye mitandao ya kijamii kuna video inayomunesha mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Jangwani Dar es Salaam, Mariana Eric Mirindima anayeeleza changamoto wanazokumbana nazo wanafunzi wanaotumia usafiri wa daladala.

"Katika video hiyo mwana-

funzi huyo alieleza kuwa baadhi ya makondakta (wahudumu) wamekuwa wakigoma kupakia wanafunzi wakidai hawalipi nauli kamili, hali inayowalazimu kusubiri usafiri kwa muda mrefu na kubaki barabarani, hali inayoathiri masomo yao," alisema Profesa Mbarawa.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari Dodoma jana, Profesa Mbarawa aliongeza: "Serikali haitavumilia vitendo vya unyanyasaji kwa wanafunzi. Haki yao ya kupata elimu kwa usalama lazima ilindwe."

Ameilekeza LATRA ihakikishe kazi ya kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu (makondakta)

kwenye mabasi inafanywa kwa kasi katika miji yote.

Ameagiza adhabu kali zitolewe kwa mujibu wa sheria kwa madereva na makondakta watakaobainika kuwanyanyasa wanafunzi.

Aidha, Profesa Mbarawa ameagiza LATRA iimarisha udhibiti wa nauli maalumu za wanafunzi, staha ya huduma na usalama wao kwa wakati wote. Ameagiza mamlaka hiyo ihakikishe treni za abiria, daladala zote na mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani zimeandikwa namba za bure ili abiria wapigie LATRA namba hizo. Namba hizo ni 0800 11 00 19 na 0800 11 00 20. Aidha, ameagiza

LATRA ishirikiane na Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushtukiza kwenye vituo vya daladala, hasa nyakati za asubuhi na jioni kuhakikisha wanafunzi wanapata usafiri.

"Niwaombe Watanzania na abiria kwa ujumla, tushirikiane kuwatetea wanafunzi wanaponyanyaswa na mtu yeyote. Mnaweza kutuma ushahidi wa picha au sauti kwa namba ya LATRA WhatsApp 0681 300 800," alieleza.

Profesa Mbarawa alisema serikali imeboresha usafiri wa wanafunzi mijini kwa kuweka mipango na mikati mbalimbali.

Aliitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuanzisha huduma za mabasi maalumu yaendayo haraka kwa ajili ya wanafunzi, hususan asubuhi na jioni. Alisema serikali imetenga mabehewa maalumu kwa ajili ya wanafunzi kwenye treni za mijini (Dar es Salaam) ili kupunguza msongamano, kuongeza usalama na kutoa unafuu wa usafiri kwa wanafunzi wanaotumia treni za mijini.

Alisema pia serikali imerasimisha na kusimamia utozaji wa nauli maalumu ya Sh 200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa.

Rungu zito makondakta wanaotesa wanafunzi

Na **MUSSA YUSUPH**, Dodoma

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kushirikiana na Jeshi la Polisi, kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vituo vya daladala asubuhi na jioni.

Amesema lengo ni kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria, makondakta na madereva wanaowanyanyasa wanafunzi.

Pia, ameiagiza LATRA kuhakikisha uthibitishaji madereva na usajili wa makondakta katika mabasi, unafanyika kwa kasi miji yote nchini.

Profesa Mbarawa, alitoka kauli hiyo jijini hapa jana, baada ya kusambaa video katika mitandao ya kijamii, ikimwonesha mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Shule ya Sekondari Jangwani, Mariana Mirindima, akiwasilisha barua yake iliyoeleza changamoto zinazowakumba wanafunzi wanaotumia usafiri wa mabasi ya mijini, maarufu daladala.

Katika barua yake, mwanafunzi huyo alieleza makondakta wamekuwa wakigoma kuwabeba wanafunzi kwa kisingizio cha kibiashara wakidai hawalipi nauli kamili.

"Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wanalazimika kusimama barabarani muda mrefu wakisubiri usafiri, wanachelewa kufika shuleni na wakati mwingine wanashindwa kabisa kufika shuleni. Hali hii inawatia hofu wanafunzi, inawachosha, inaathiri masomo na usalama wao kama watoto.

"Wanafunzi wanategemea sana daladala kama njia yao kuu ya usafiri, wanapoachwa njiani au kunyimwa huduma wanakuwa kwenye mazingira hatarishi na kunyimwa haki yao ya msingi ya kupata elimu kwa usalama," alieleza Profesa Mbarawa.

Alisema katika kukabiliana na changamoto za usafiri wa abiria wakiwemo wanafunzi, serikali imeweka mipango na mikakati mbalimbali.

Aliitaja mikakati hiyo ni kuanzisha huduma za mabasi maalumu yaendayo haraka kwa ajili ya wanafunzi, hususan asubuhi na jioni, kuhakikisha wanafunzi wanafika shuleni na kurejea nyumbani salama kwa wakati.

"Kutenga mabehewa maalumu ya wanafunzi kwenye treni za mijini (Dar es Salaam) hatua inayolenga kupunguza msongamano, kuongeza usalama na kutoa unafuu wa usafiri kwa wanafunzi wanaotumia

treni za mijini.

Aliongeza: "Kurasimisha na kusimamia utozaji wa nauli maalumu ya sh. 200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala. Hatua hii, inalenga kuhakikisha wanafunzi wanapata huduma kwa gharama nafuu, kutekeleza sheria na kanuni za kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu (makondakta) wa vyombo vya usafiri wa umma, mabasi na treni."

Hata hivyo, Profesa Mbarawa aliiagiza LATRA kuhakikisha uthibitishaji madereva na kusajili wahudumu (makondakta) katika mabasi unafanyika kwa kasi miji yote nchini na kutoa adhabu kali kwa mujibu wa sheria kwa madereva na makondakta watakaobainika kuwanyanyasa wanafunzi.

Vilevile, aliagiza kuimarisha udhibiti wa nauli maalumu za wanafunzi, staha ya huduma na usalama wao kwa wakati wote, kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma, watumia huduma wajue haki na wajibu wa kila mmoja, huku akiitaka LATRA kushirikiana na Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye vituo vya daladala hasa asubuhi na jioni kuhakikisha wanafunzi wanapata usafiri.